MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI OKTOBA, 2026 NA MWELEKEO KWA MWEZI NOVEMBA, 2026.

Dondoo za tathmini ya Oktoba, 2026 na mwelekeo wa Novemba, 2026:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Oktoba, 2026 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto kwa mwezi Novemba, 2026 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2026 vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ikiashiria kuanza kwa mvua za Vuli, 2026 katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria.

ii. Hali ya joto la wastani hadi la juu ilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi, hususan maeneo yaliyopata mvua chache, ikiwemo maeneo ya ukanda wa pwani.


iii. Katika mwezi wa Novemba 2026, mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (unimodal). Aidha, mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza na kuimarika katika maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki na ukanda wa pwani ya kaskazini.

1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2026.

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2026, vipindi vya mvua vilivyoambatana na ngurumo za radi, vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya Bonde la Ziwa Victoria. Hali hii iliashiria kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli 2026, kama ilivyotabiriwa. Aidha, mvua zenye mtawanyiko usioridhisha zilijitokeza katika maeneo ya ukanda wa pwani.

Kuelekea mwishoni mwa mwezi, baadhi ya vituo vya hali ya hewa vilianza kurekodi vipindi vya mvua vilivyoambatana na upepo mkali. Kiasi kikubwa zaidi cha mvua kwa siku cha milimita 57.7 kilirekodiwa katika kituo cha Tanga mnamo tarehe 31 Oktoba 2026, kikifuatiwa na milimita 52.6 zilizorekodiwa katika kituo cha Mlingano siku hiyo hiyo.

Vituo vingine vilivyorekodi kiasi cha mvua cha milimita 30 au zaidi vimeoneshwa hapa chini.



Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 30 au zaidi katika mwezi Oktoba, 2026

2.0 MWELEKEO KWA MWEZI NOVEMBA, 2026

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la Bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, ikiashiria kuanza kuimarika kwa hali ya El Niño. Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi, karibu na Pwani ya Afrika mashariki, linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, wakati eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la bahari la chini kidogo ya wastani hadi wastani. Hali hii inatarajiwa kuongeza upepo

wenye unyevu kuvuma kuelekea ukanda wa pwani ya nchi yetu na mikoa ya jirani. Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki, karibu na pwani ya Angola linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani hadi wastani.

Kwa upande mwingine, joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (kusini mwa kisiwa cha Madagascar) linatarajiwa kuendelea kua la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kudhoofisha mgandamizo mkubwa wa hewa wa Mascarene na hivyo kupunguza kasi ya upepo wenye baridi unaovuma kutoka kusini kuelekea katika maeneo ya nchi yetu.

2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2026

Katika kipindi cha mwezi Novemba 2026, mvua za Vuli zinatarajiwa kuendelea na kusambaa katika maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki na ukanda wa pwani ya kaskazini. Wakati huohuo, mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika maeneo ya kusini mwa nchi.

Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi inatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan maeneo yanayotarajiwa kupata upungufu wa mvua.

Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne kwa baadhi ya maeneo haya.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan maeneo yenye miinuko.

Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya pili na ya nne ya mwezi Novemba.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya pili na ya nne ya mwezi Novemba.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):

Vipindi vya mvua kwa baadhi ya maeneo vinatarajiwa. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya pili na ya nne ya mwezi Novemba.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kwa baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya pili na ya nne ya mwezi Novemba.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):

Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache hususan kuelekea mwishoni mwa mwezi.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):

Vipindi vifupi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususani kuelekea mwishoni mwa mwezi.

2.3 MATARAJIO KWA MWEZI DESEMBA, 2026

Katika kipindi cha mwezi Desemba 2026, mvua za Vuli zinatarajiwa kuendelea na kuimarika kwa mtawanyiko wake katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.

Kwa upande mwingine, mvua za Msimu katika maeneo ya magharibi, nyanda za juu kusini magharibi, maeneo ya kusini, kanda ya kati na pwani ya kusini zinatarajiwa kuendelea, hali itakayochangia kuongezeka kwa mvua katika maeneo mengi ya nchi.

2.4 USHAURI

Mvua za msimu zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza. Hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko mara kwa mara au jirani na maeneo hayo wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mvua kubwa ikiwemo hatari ya mafuriko.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

Imetolewa tarehe 01 Novemba, 2026 na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.